

**Riport ya mafunzo ya usalama kwa wapanda baisikeli kwa kuzijua sheria za
usalama barabarani**

Tarehe 6 juni 2009 na tarehe 13 juni 2009

Walimu walioshiriki kufundisha ni:

Kibwana Mohamed

Juma S Jongo

Dominata Rwechungura

Mussa Omary

Hamad Bwaja

Filbert Mbecha

Mafunzo yetu yalijumuisha jumla ya wapanda baisikeli ishirini na tano (25) wakiwemo walemavu. Ni mafunzo yaliyo walenga raia. Mafunzo yalitolewa kwa hazaria na kwa vitendo nje ya darasa. Washiriki wote walipata huduma ya chai na chakula cha mchana kwa siku zote walizoshiriki mafunzo.

Pia washiriki walipewa nafasi ya kujadili kuhusu malengo ay miaka mitano ijayo kwa makundi, na kila kundi lilipewa lengo moja kujadili. Lengo ni kuwa pima kama wameelewa kuhusu hilo.

Na siku ya mwisho wa mafunzo yetu walimu tulimkaribisha mgeni rasmi Diwani wa Kata ya Makulumla Ndugu Rajabu Hassani. Kabla ya kuaribishwa kutoa zawadi, Mw Rwechungura alitoa maelezo mafupi kuhusu UWABA, kazi zake na malengo yetu. Na baada ya hapo alikaribishwa kuwazawadia wahitimu wa mafunzo vyeti kofia helmet na reflector jacket.

Alitoa hotuba fupi kwa wahitimu wa mafunzo. Na hii ni nukuu ya hotua yake:

Matatizo wanayo kumbana nayo wapanda baisikeli ni kuzalauliwa na madereva wa magari, kwa sababu ya kutojua sheria na haki zetu. Lakini kupitia mafunzo haya ni moja ya changamoto kwa wahusika wakiwemo traffic police, serikali, TANROADS n.k.

Kwa hiyo alifurahi kualikwa kwani ni changamoto kwake kuitakikisha suala la baisikeli ni moja ya agenda katika mikutano yao.

Faida za baisikeli: pia alisema kwamba baisikeli hukuinga na kukuondolea magonjwa kama vile kisukari, presha, koresto n.k.. Alisema yeye ni mmoja wa watu ambao walikuwa na sumbuliwa sana na magonjwa hayo lakini baada ya kushauliwa na daktari atumie baisikeli na sasa yupo safi sana tena magonjwa hayo.

Vile vile alisema baisikeli hupunguza ajali, msongamano na alisema baisikeli ni chombo cha kwanza cha usafiri katika familia kwa sababu ni bei nafuu.

Pia aliambatana na diwani wa kata ya manzese Ndugu Eliam Manumbu yeye alipongeza kazi zetu UWABA na uongozi kwa ujumla na alisema baisikeli husaidia kiuchumi hasa gurudumu tatu (guta) hutoa ajira kwa vijana kwa hiyo aliunga mkono suala la baisikeli asilimia mia moja. Pia alitoa wazo kwamba kuna umuhimu wa kuwa na bima na leseni kwa wapanda baisikeli.

Changamoto tuliyopata walimu:

Washiri walikuwa makini na walikwa wadadisi wa maswali kwa lengo la kutaka kuelewa zaidi. Pia tuliweza kupata ufafanuzi mzuri kwa maswali yaliyohusu michezo kutoka kwa Alen J Nyanginywa katibu wa Chama cha Baisikeli Dar es Salaam (CHABADA).

Pia tulishauliwa ni vizuri kuweka onyo nyuma ya reflector jacket kwa madereva ili kuachiwa nafasi ya mita moja au moja na nusu.

Vile vile ni muhimu abiria naye avae helmet kwa usalama kwa hiyo ni muhimu kuwa na helmet ya akiba kwa ajili ya abiria.

Pia ni muhimu kuwa na bima.

Mwisho wa riport.

Riport hii imeandaliwa na walimu wote walioshiriki kutoa mafunzo na kuandikwa na Mw Filbert Mbecha.